035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
A. waraka
B. barua maalum
C. barua ya kiofisi
D. Barua rasmi

Jibu sahihi ni **D**

**Katika karatasi ya majibu:**

2. [A] [B] [C] [D] 12. [A] [B] [C] [D] 22. [A] [B] [C] [D] 32. [A] [B] [C] [D] 42. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

Contact Mr Machuki 0724333200/0795491185 for Marking Schemes or kenyaeducators.co.ke

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

___1___ huwa chanzo cha mema na maovu. Wasemao ___2___ kuwa ulimi ni kiumbe kidogo ___3___ matatizo yake ni makubwa. ___4___ kama hakitatumiwa inavyofaa kinaweza kusababisha ___5___ ambayo inaweza kuteketeza ulimwengu mzima. Mtu ambaye ___6___ uhakika kuhusu namna ya kuutumia ulimi wake ni afadhali ___7___ kabisa. Kabla ya kufungua kinywa kusema au kuchukua kalamu kuandika neno, ni sharti ___8___

1. A. Blanketi la babu lisiloraruka B. Blanketi la Mungu lililojaa chawa kochokocho
   C. Blanketi langu lenye madoadoa D. Boga langu zuri lakini halikomai

2. A. hawasemi B. wanasema C. wasemao D. husema

3. A. na B. lakini C. isipokuwa D. hila

4. A. Kiumbe huyu B. Maumbile haya C. Kiumbe hiki D. Umbo hili

5. A. matatizo B. tatizo C. mioto D. moto

6. A. ana B. anajua C. hajui D. hana

7. A. kunyamaa B. kunyamanza C. kunyamasa D. kukimia

8. A. kuhatari kabla ya hatari B. kutahadhari kabla ya hatari
   C. kuvuta subira kabla ya hatari D. kujihatarisha kabla ya hadhari

Kijana Sadala ___9___ akiishi katika kitongoji cha Kibra jijini Nairobi. Malezi yake yalikuwa tofauti ___10___ yale ya watoto wengine. Tabia zake zilikuwa ___11___ hadi yeye na wazazi wake walipohamia katika ___12___ mapya pale Lavington. Pale hapakuwa na wasena wenye hulka ___13___. Kwa hivyo aliendelea kuboresha nidhamu yake zaidi. Watu wa mahali pale ___14___ sana familia hii ya bwana Ibrahim. Moyo wao ___15___ ndio uliowafanya kufikia upeo wa mafanikio yao.

9. A. alikua B. hakuwa C. alikuwa D. halikua

10. A. kwa B. kama vile C. na D. kwa vile

11. A. mzuri B. mbaya C. mbovu D. nzuri

12. A. nyumba B. makaazi C. makazi D. wakazi

13. A. muwi B. mbi C. mzuri D. nzuri

14. A. waliwaenzi na kuwapenda B. waliwaambua na kuwatelekeza
    C. waliwapenda na kuwachukia D. walipenda na kuienzi

15. A. insafu B. kidogo C. mbaya D. mdogo

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.*

16. Ni sentensi gani inayounganisha vifungu hivi viwili?

**Jomba ni mzee. Jomba anakimbia kwa kasi**

A. Jomba anakimbia kwa kasi minghairi ya yeye ni mzee

B. Jomba ni mzee maadamu anakimbia kwa kasi

C. Jomba anakimbia kwa kasi licha ya kuwa yeye ni mzee

D. Jomba ni mzee madhali anakimbia kwa kasi

17. Neno '**chawa**' lina herufi ngapi tofauti za Kiswahili?

A. 3

B. 5

C. 4

D. 2

18. Tambua sentensi inayoonyesha hali ya kutendesha

A. Kamishna wa polisi ametangaza vita dhidi ya dawa za kulevya

B. Mwamba ngozi amekaza kamba ili ikauke kwa haraka

C. Kumbe ni wewe unayemliza mtoto wangu mara kwa mara

D. Chakula hicho kilimtosha mtoto wa shangazi

19. '**Ki**' imetumikaje katika sentensi ifuatayo?

**Mbwa huyo akimwona ajinabi atamrukia kijeshi**

A. Masharti, nomino

B. Wakati, nomino

C. Masharti, kielezi

D. Wakati, namna

20. Andika kwa msemo wa taarifa:

**"Nilimpigia shangazi yako simu jana."**

**Mama alimwambia mwanawe**

A. Mama alimwambia mwanawe kuwa alikuwa ampigie shangazi yake simu jana

B. Mama alimwambia mwanawe kuwa alikuwa amempigia shangazi yake simu siku iliyopita

C. Mama alimwambia mwanawe, "Nilimpigia shangazi yako simu jana."

D. Mama alimwambia mwanawe kuwa alimpigia shangazi yake simu siku iliyofuata

21. Watu wengi ________ hupenda kusafiri mchana kujionea mandhari ya nchi

A. aghalabu

B. kaifa

C. angalau

D. angaa

22. Chagua sentensi ambayo haikuendelezwa sahihi kimantiki

A. Amejipaka mafuta usoni mwake

B. Wanafunzi wengi waliwahi shuleni

C. Mabata wanapenda kuchezea vidimbwini

D. Ajali nyingi zinaweza kukingika

23. Tambua sentensi iliyo na 'po' ya wakati

A. Nilipowasili wanakwaya walikuwa wakiimba

B. Hatukufahamu walipoishi watu wa jamaa yetu

C. Nilipolala palikuwa na baridi kali

D. Tutakapowasili tutalakiwa kwa shangwe

24. **Jiti lile lilipigwa na radi.**

Wastani wa sentensi hii ni

A. Mtu yule alipigwa radi

B. Mti ule ulipigwa na radi

C. Kijiti kile kilipigwa na radi

D. Ujiti ule ulipigwa na radi

25. Chagua **ukanusho** wa

**Mama amepika chakula kikapikika**

A. Mama hajapika chakula wala hakikupikika

B. Mama hajapika chakula wala hakijapikika

C. Mama hakupika chakula na hakikupikika

D. Mama hakupika chakula na hakijapikika

26. Ni sentensi gani iliyo katika hali ya kuagiza?

A. Mkija mapema nitawepeleka uwanjani

B. Mwakio ulisikiliza wimbo akujua kuimba.

C. Nisaidieni kuinua mzigo huu mzito

D. Tulimpata akiwa anapika pilau

27. Ni nini maana ya msamiati **kupiga mnada**?

A. Kuuza kwa kuongeza bei

B. Kuuza kwa kushindania bei

C. Kuuza kwa rejareja

D. Kuuza kwa kukopesha

28. Jibu **kitendawili**: Mimi daima hutembea na nyumba yangu

A. Kobe

B. Mjusi

C. Nyoka

D. Nyuki

29. Je, utamwitaje mtoto wa binamu?

A. Mbiomba

B. Mjukuu

C. Umbu

D. Mpwa

30. Mama alisema kuwa angerejea mtondogoo. Iwapo ilikuwa siku ya Jumamosi mosi, je, anatarajiwa kurejea siku gani na tarehe ngapi?

A. Jumapili tarehe mbili

B. Jumatano tarehe tano

C. Jumatano tarehe nne

D. Jumanne tarehe nne

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31- 40***

Nilizaliwa katika familia ya walalaheri. Nyumbani kwetu palikuwa na kasri kubwa la ghorofa ambalo lilikuwa limepambwa likapambika. Weupe wake uling'aa upande wa juu ambao haukukigwa na ua wa mawe mzuri. Sifa za familia yetu zilikuwa zimezagaa kotekote. Utajiri wetu haukuwa wa mali tu. Nina na abu walikuwa na utajiri pia na roho insafu. Waliwaruzuku na kuwafaa wengi. Walalahoi waliohitaji msaada hawakuchelea kufika kwetu nyumbani. Petu palikuwa pa wageni wa kila siku, saa, dakika na sekunde. Binafsi, nilikuwa nikipenda sana kutangamana na watu. Kuna wale waliofika, wakala, wakashiba na hata wakalala kwetu. Watu wa kaya yetu walimrai baba kuwania ugavana. Walikula yamini kuwa kura zote zingekuwa zake. Baba hakupenda siasa. Kwa hivyo alikana kwa kinywa na roho. Alijua kuwa nyoyo za wanasiasa zilikuwa tititi na hakutaka kubadilisha hulka yake ya utu. Njenje alikuwa nazo alhamdulilahi.

Muda ulisonga kwa kasi na nikajipata nikiwa katika shule ya msingi. Mnuna wangu ambaye alikuwa bado chekechea, hakuwapenda wageni kwani <u>aliwabugudhi na kuwaita waegemea nundu</u>. Abu hakusita kumwonya dhidi ya tabia hiyo hasi. Baba alinitia motisha nitie bidii shuleni. Yeye alikuwa mchapa kazi enzi zake zote na hakutaka ugoigoi hata kidogo. Japo tulikuwa na kila kitu, mbali na watu wengine wenye haiba kama yetu, hatukudekezwa kamwe. Ungefanya ugoigoi baba angechukua bakora na kukutandika kijeshi. Tuliamua kufuata nyayo zake. Tulielewa fika kuwa mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina. Baada ya kuufanya mtihani wangu wa kitaifa, niliungojea kwa hamu na ghamu. Nilikuwa na mchanganyiko wa mawazo kuhusu kupasi na kuanguka. Baada ya matangazo kufanywa, baba alifika nyumbani akiwa amebeba gazeti la 'Mzalendo.' Cha ajabu, picha yangu ilikuwa upande wa mbele. Alinipiga pambaja na kunishukuru kwa ubingwa wangu.

Ualishi wangu katika shule ya upili ya mtakatifu Yosefu ulikaribishwa kwa shangwe na vigelegele. Nilipolitia guu langu katika shule ile, tabia zangu zilianza kuwa na nyufa. Kwa hakika, sikuona utakatifu wowote katika shule hii. Nilimpata rafiki, Mfaki ambaye alinifanya kukanyaga chechele. Nigeuka nikawa bendera inayofuata upepo. Daima tuliandamana na Mfaki. Mwanzoni alionekana kunipa motisha nitie bidii masomoni. Mfaki alikuwa wembe kama mimi. Tabia yake kamili ilijitokeza tu pindi muda ulivyoendelea kusonga. Nilitaka kumwacha lakini ushawishi wake ulikuwa wa kipekee. Kila wakati, alinileteа udohoudoho- vitu vitamu vitamu. Mlachake majali, nikabadilika na kuwa kitu tofauti.

Siku moja, Mfaki alifika chumbani mwangu usiku. Alisema kuwa alikuwa amekuja kunijulia hali. Alinipatia aina fulani ya unga na akaniambia nionje. Nilichelea lakini nikashawishika kuonja. Niliulamba unga ule. Nilihisi uchangamvu fulani. Nilimwambia nilivyohisi halafu akakenua. Alinieleza kuwa unga huo humsaidia sana wakati wa mtihani. Baadaye alinionyesha mzee fulani ambaye angenyemelea ua wa shule na kuuza. Baada ya kulala na kuamka siku iliyofuata, nilihisi nikiwa mgonjwa. Nguvu zilikuwa zimeniishia na kichwa kuniwanga. Nilifahamu fika kuwa uchangamvu ule ulikuwa ni wa mkakasi tu. Nilianza kujilaumu 'laiti' ningalijua. Tindi moja, tindi mbili, tindi tatu, nikawa mraibu wa dawa za kulevya.

Siku ya nyani kufa, miti yote huteleza. Asubuhi moja niliamka nikajikuta nikiwa kwenye kichumba kimoja baridi. Hapakuwa na dirisha na mlikuwa na baridi shadidi. Baadaye nilifunguliwa na mwalimu mkuu. Nilielezewa yaliyojiri siku ambayo ilitangulia na nikashangaa. Niliambiwa kuwa niliokotwa barabarani nusura nikanyagwe na gari! kengele ilikirizwa na nikaanikwa paruwanja gwarideni. Tahayuri ilinivaa si kidogo. Nilizomewa na hedimaster huku wanafunzi wenzangu wakicheka kwa kwa kwa. Jambo la ajabu ni kuwa, Mfaki alikuwa gwarideni huku akicheka kwa sauti ya bezo na dharau. Nilifukuzwa nyumbani nije na mzazi baada ya wiki mbili.

Siku ya kurudi nilikuwa nimeteseka vya kutosha. Niliamua kuungama mbele ya wazazi wangu na mwalimu mkuu kuwa nimeokoka na kuongoka. Mama yangu alinipa ushauri nasaha. Niliamua kuwa balozi wa kupiga mihadarati shuleni mwetu. Mtu wangu wa kwanza niliyeweza kubadilisha alikuwa ni Mfaki. Ama kwa hakika INAWEZEKANA!

31. Kulingana na aya ya kwanza tunaweza kusema kuwa
A. familia ya Majali ilikuwa na utajiri wa mali tu
B. hakuna wakata walioruhusiwa kutalii kwao
C. mbali na kuwa na ulalahai, Majali aliwafaa waliokuwa na shida
D. msimulizi alikuwa akichoshwa na wageni waliojaa kwao

32. Unafikiri ni kwa nini Majali hakutaka kuwa mwanasiasa?
A. Alikuwa na mali mengi kuliko wanasiasa wote
B. Alipendelea kutangamana na maskini kuliko wanasiasa
C. Kulikuwa na watu wengi waliofika kwake, kula na kulala
D. Hakupendelea kamwe kugeuka na kuwa mroho kama wanasiasa

33. Ni mambo yapi yanayoonyesha kuwa Majali alikuwa na utajiri wa pesa na roho?
A. Kukidhi mahitaji ya wanawe na kuwapa watu ruzuku
B. Kukithi mahitaji ya watu wengine kuliko watu wa kwake
C. Kuyakithi mahitaji ya wana na watu kufurika kwake
D. Kuyakithi mahitaji ya wanasiasa wote

34. Ni tabia gani zinazosemekana kuwa na matajiri wengi ambazo Majali hakuwa nazo? Matajiri wengine;
A. hawakuruhusu watu kwenda kwao ovyo ovyo
B. hawakuwa na moyo wa kuwasaidia watu kama Majali
C. waliwadekeza wanawe kinyume na Majali
D. hawakuwa na moyo insafu kama Majali

35. Kifungu *"...aliwabugudhi na kuwaita waegemea nundu"* Inaonyesha kuwa ndugu mdogo alikuwa
A. mwenye majisifu
B. mwenye uzushi
C. mwenye mapuuza
D. mwenye uchoyo

36. Ni kwa nini msimulizi wa makala haya alisoma kwa bidii?
A. Alikuwa akiyapenda masomo yake kutoka utotoni
B. Kwa sababu baba yake alikuwa mkali ja simba
C. Baba yake ndiye alikuwa kioo chake cha bidii
D. Alitaka kufuata nyayo za baba na ndugu yake

37. Ni kwa nini Mlachake Majali alishidwa kumwacha Mfaki?
A. Alikuwa akimpenda kwa dhati
B. Mfaki alikuwa na ushawishi usiomithilika
C. Mfaki alikuwa mwerevu kama alivyokuwa msimulizi
D. Mfaki alikuwa amemwojesha unga mtamu

38. Mambo yanayoonyesha kuwa kifungu hiki kinapinga matumizi ya dawa za kulevya ni
A. msimulizi kufukuzwa shule, msimulizi kujiunga na wanaopinga matumizi mabaya ya dawa za kulevya
B. kufunzwa uraibu na rafiki yake, kujulikana na kutumwa nyumbani
C. mwalimu kumshauri msimulizi, wazazi wake kumwonya msimulizi shuleni
D. walimu kugundua tatizo la msimulizi, msimulizi kuaibika shuleni

39. Ni jambo gani linalotia moyo zaidi mwishoni mwa makala uliyoyasoma?
A. Mfaki kufanikiwa kumwadaa mwana wa Majali
B. Mwana wa Majali kuokoka na kuongoka
C. Wazazi na mwalimu kumshauri mwana aliyepotoka
D. 'Mwalimu' wa mihadarati kuokoka na kuacha mihadarati

40. Methali ambayo haifai kujumlisha ujumbe wa taarifa hii ni
A. Nazi mbovu harabu ya nzima
B. Mchezea tope humrukia
C. Mwegemea nundu haachi kunona
D. Mchovya asali hachovyi mara moja

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41- 50***

Amani ni hali ya kuwa na utulivu bila vita. Taifa ambalo limezoea kujivunia amani kwa miaka mingi hawajui hasara inayoletwa na vita. Kuna msemo wa kale uliosema kuwa amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Ningependa kusema kuwa, msemo huu si wa kweli nyakati zote. Kimsingi ni kwamba amani inaweza kupatikana kwa njia ya mashauriano na maafikiano. Ukiutumia upanga unaweza kumjeruhi au kumwua mwenzako. Sasa amani itakuwaje wakati ambapo 'adui' yako ameishia akhera? Njia ya mashauriano na maafikano ndiyo dawa mujarab ya amani.

Vita wakati wote huleta hasara isiyomithilika. Gharama na hasara ya vita ni kubwa na kuziba magofu yanayoletwa na vita yanaweza kuchukua muda mrefu sana kuziba. Tukitaka kuyajua maafa yaletwayo na vita hususan katika ukanda wa Afrika mashariki, tuna mifano maridhawa. Hebu vuta darubini na ukumbuke vita pale Rwanda kati ya 1992 na 1994. Tazama nchi ya Sudan ilivyochelewesha maendeleo kwa sababu ya mizozo isiyokwisha. Nchi ya Somalia daima inatetereka kwa kukosa amani. Vita vinaweza kuzusha viongozi, uharibifu wa mali, hali ya utulivu hutokomea na furaha na maendeleo hupotea kama vile moshi. Wanenao hunena, <u>*kama hujui kufa tazama kaburi*</u>. Sizungumzii taifa letu kati ya 2007 na 2008.

Sasa hebu tazama shida zinazotokana na vita. Vurugu zinapotokea watu hutoroka, kila mmoja akikimbia kusalimisha roho yake. Wakati kama huu, mali kama vile mashamba, majumba ya kifahari, magari mengi, pesa na hata mifugo huwa mizigo mizito isiyobebeka. Katika hali hii, familia hujikuta zimesambaratika. Upweke nau huzidi. Pa kukimbilia pia huwa shida. Hali ya utegemezi huibuka. Wakimbizi hutegemea usalama kutokana na ukarimu na ukaribu uliopo kati yao na wahisani wao. Mambo hayawi sawa hata kidogo. Wakati mkimbizi hana uhuru nchi au mahali anapokaa huwa kama nguo ya kuazima ambayo haisetiri matako.

Unapokuwa katika hema ya ukimbizi ndipo utatafakari na kukumbuka umuhimu wa amani. Hapa ndipo mja hujuta na kukumbuka mambo yasiyo na msingi yaliyozua ghasia. Wengi hukumbuka vurumai kubwa zinazotokana na tofauti za kisiasa, kiuchumi na kikabila, ufisadi na tamaa. Wengine huwaza kwa uchungu kuhusu hali ya mali zao walizochuma kwa miaka mingi kuangamizwa kwa sekunde moja tu. Wengi wao hutatizika kimawazo na kuwa na shida za akili ambazo zinaweza kuwaathiri kwa muda mrefu baada ya vita. Kukari kuntu, vurumai nyingi husababishwa na tofauti za kugombania ukuu na uongozi.

Ukimbizi wa nje na ndani huleta karaha tele; husababisha kidonda ambacho, hata kama kitaonekana kupona, uchungu wake haukwishi kamwe. Wakimbizi mara nyingi hulilia mahitaji muhimu kama vile: chakula, maji, makao, mavazi na malazi. Magonjwa hatari pia hayakosi kulipuka kila mara. Kwa kuutia msumari kwenye kidonda, vifo pia huzidi. Sio kutoka kwa maradhi tu ila pia kutokana na mapigano na dhiki za kisaikolojia. Uvunjaji wa sheria huzidi na uchumi huzorota kwani hata watalii huchelea kuingia.Hapa nchi hupoteza pesa nyingi za kigeni zinazotokana na wageni hawa. Umaskini nao hulikodolea taifa macho. Kwa kawaida wakimbizi hukosa heshima na ustaarabu wao.

Wanaoathirika sana kutokana na vita huwa wananchi wa kawaida. Si viongozi na matajiri. Ili kuhakikisha kuwa jamii zote zinaishi kwa amani, haifai kungojea serikali, wazazi na walimu eti ndio watakaotusaidia. Ni jukumu la kila mmoja kujaribu kuibua na kukuza hisia za kizalendo miongoni mwa wanajamii. Taifa nalo liwaelimishe watu wake kuhusu umuhimu wa amani.

41. Kwa mujibu wa aya ya kwanza ni kweli kusema kuwa

A. amani haiji ila kwa ncha ya upanga

B. amani huimarishwa zaidi baada ya maafikiano

C. gharama ya vita hupungua kwenye amani

D. amani huwezesha watu kujifunza mengi

42. Unafikiri ni kwa nini mwandishi hashabikii msemo "*amani haiji ila kwa njia ya upanga*"?

A. Upanga mara nyingi huleta maafa na magovu

B. Ni msemo usiokuwa na ukweli hata kidogo

C. Ni sharti watu watengamane ndipo tupate amani

D. Maafa husababisha watu kushauriana na kuafikiana

43. Ni muda gani umepita tangu taifa la Rwanda lianze kukumbwa na vita hadi sasa kulingana na ufahamu?

A. Zaidi ya miaka ishirini na miwili

B. Karibu miongo miwili

C. Miongo ipatayo ishirini na miwili

D. Miaka kumi na miwili

44. "*Kama hujui kufa tazama kaburi*" ina maana kuwa

A. kama hujawahi kuyaelewa matatizo, chunguza chanzo chake

B. kama hujawahi kukielewa kifo chunguza kiini chake

C. kama hujui yanayoletwa na kifo hebu jaribu kufa

D. kama hukielewi kifo hebu tazama matokeo yake

45. Maafa haya yote husababishwa na vurungu kulingana na aya ya tatu ila

A. usetiri wa mali kama vile; mashamba, majumba na magari

B. kusambaratika kwa familia nyingi

C. upweke na umaskini hushamiri

D. husababisha kuwepo kwa wakimbizi wanaokosa uhuru

46. Kiini hasa cha kusababisha vita hususan katika mataifa ni nini kulingana na habari?

A. Ukabila

B. Siasa

C. Ufisadi

D. Tamaa

47. Wakimbizi hutegemea hasa

A. utu wa wenyeji wao

B. urafiki wa wenyeji

C. maslahi ya taifa lao

D. utu wa wao kwa wao

48. Ukimbizini

A. nchi hupoteza pesa za kigeni

B. uchumi wa nchi huzorota

C. shughuli za kuzalisha chakula hozorota

D. waathiriwa hupoteza hadhi zao

49. Ni kitu gani kikubwa kinachoikumba nchi kutokana na vita kulingana na taarifa?

A. Nchi kupoteza walinda usalama

B. Nchi kukumbwa na tatizo la kimawazo

C. Nchi hupoteza pesa za kigeni

D. Nchi hukumbwa na tatizo la wawekezaji

50. Jukumu la kudumisha amani

A. linahitaji ushirikiano wa walimu na viongozi

B. linahitaji ushirikiano wa raia wote

C. linahitaji kushughulikiwa na serikali husika

D. linahitaji kushughulikiwa na wahisani wa wakimbizi

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako**

***Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukianza kwa kifungu ulichopewa.***

*Kama si mwalimu wangu wa ushauri nasaha, kwa hakika singekuwa nilivyo sasa...............*